# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL5

# KISWAHILI PAPER 1 ANSWERS

**Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.**

**1. - Hii ni ripoti.**

**- Muundo wa ripoti rasmi izingatiwe.**

**-Kichwa: -kiwe na herufi kubwa.**

**-Utangulizi.**

**- Historia fupi ya suala linalotafitiwa itolewe ikiwa ni pamoja na kutaja wanajopo watano na muda wa kutafiti.**

**-Yaliyoshughulikiwa.**

**- Taratibu za kufanyia utafiti ziorodheshwe.Hizi ndizo zitafuatwa baadaye katika mwili wa insha.**

**- Mwili/matokeo ya uchunguzi.**

**- Ni maswala yaliyoshughulikiwa na jopo pamoja na utaratibu uliofuatwa kutafiti yale yalioangaziwa.**

**- Matatizo.**

**- Iwapo jopo lilikumbana na matatizo yoyote,matatizo hayo yaorodheshwe chini ya kijianwani cha matatizo.**

**- Hitimisho.**

**- Sifa za ripoti zirejelewe.**

**-Mapendekezo.**

**- Jopo litoe msimamo wake baada ya kukamilisha utafiti.**

**-Jina,sahihi na cheo cha mtayarishi pamoja na tarehe ziandikwe. Tanbihi:**

**- Mtahiniwa asipofuata sura ya ripoti rasmi,aondolewe alama 4**

**Vidokezo**

**Sababu za udanganyifu**

**1) Kukosa kujiandaa ipasavyo kabla ya mtihani.**

**2) Uzembe wa wanafunzi katika kujiandaa masomoni.**

**3) Baadhi ya wazazi huwa wakali sana kwa watoto wao wasiofanya vyema masomoni.**

**4) Wazazi wengine kutaka watoto wao wajiunge na vyuo vikuu kwa njia yoyote ile.**

**5) Ufisadi kuwa wa hali ya juu kiasi kwamba walioaminiwa kuweka siri katika mmtihani huhongwa na kutoa nakala za mtihani hiyo.**

**6) Ni njia ya kuchumia mali kwa watu wengine kwani soko itayari ya mtihani.**

**7) Mashindano miongoni mwa shule.**

**8) Wakuu wengine kutaka sifa baada ya matokeo ya mtihani.**

**9) Limekuwa kama jambo la kawaida katika baadhi ya maeneo fulani.**

**10) Teknolojia mpya-matumizi ya simu na mtandao.**

**Madhara ya udanganyifu:**

**1) Matokeo ya mtihani kwa jumla kuathiriwa vikali kwani viwango vingine vya alama huwekwa juu sana.**

**2) Watu wengine huishia jela kwa kujihusisha na udanganyifu huu.**

**3) Watahiniwa waliohusika kukosa matokeo ya mtihani.**

**4) Wanafunzi wasio na hatia huathirika kwa matokeo ya mtihani.**

**5) Kukosa Imani kwa taasisi ya kushughulikiwa mitihani nchini (utunzi na usahihishaji)**

**6) Wasiostahili kujiunga na vyuo vikuu na kuwanyima haki wanaostahili.**

**7) Mitihani bandia kuingia sokoni kwa madai kuwa ni ya kweli.**

**8) Matokeo mabaya baada ya kudanganya hufanya wanafunzi wengine kujitoa uhai.**

**Jinsi ya kukabiliana na udanganyifu (suluhisho)**

**1) Wanafunzi walenge kupata alama kulingana na uwezo wao.**

**2) Wazazi wawe na matarajio ya matokeo ya mtihani kulingana na uwezo wa watoto wao.**

**3) Shule zishindane kulingana na kiwango chao masomoni.**

**4) Walimu watayarishe watahiniwa vilivyo.**

**5) Mfumo wa elimu ufanyiwe marekebisho ili usiegemee kupita mitihani pekee,bali uangazie vipawa vya wanafunzi katika nyanja zingine k.v michezo,sanaa,nyimbo n.k.**

**6) Wasimamizi wa shule,mtihani na walimu kwa jumla wawe macho wakati wa mtihani.**

**7) Hatua kali zichukuliwe kwa wale watakaojihusisha na udanganyifu.**

**Tanbihi:**

**Zingatia hoja zingine za watahiniwa**

**2. Tatizo la usalama nchini Kenya ni janga la kujitakia.Jadili.**

**- Usalama nchini.**

**i) Insha ya mjadala.**

**ii) Mtihiniwa atoe hoja za pande mbili.**

**iii) Mtahiniwa ahitimishe hoja nyinyi au katikati iwapo hoja zitatoshana kiidadi.**

**Maudhui.**

**a) Kuunga mkono.**

**i) Utepetevu wa walinda –usalama.**

**ii) Maafisa wa usalama wa Kenya kuingia Somali na Al-Shabaab.**

**iii) Kutosomesha watoto.**

**iv) Raia kutowajibika kuwafichua wahalifu.**

**v) Mihadarati.**

**vi) Tamaa.**

**vii) Malipo duni kwa walinda usalama.**

**viii) Umaskini.**

**ix) Ukabila.**

**b) Kupinga.**

**i) Uchache wa walinda usalama.**

**ii) Ni tatizo la kimataifa kama vile mafuriko,radi,maporomoko ya ardhi.**

**iii) Umaskini.**

**3. Swali la methali.**

**Uzuri wa mkakasi,ndani kipande cha mti.**

**Maana ya mkakasi:**

**1. Mti mrefu na laini sana.**

**2. Chombo cha mviringo amabacho kwa ndani huzungushiwa mbao na hutumiwa kuwekea vitu vidogo vidogo.**

**Mtahiniwa atunge kisa kinachoafiki methali kwamba uzuri wa nje hauwezi kukifanya kitu kiwe chema,wa ndani una umuhimu zaidi**

**4. - Lazima mtahiniwa amalize kwa maneno haya.**

**-Asipomaliza kwa maneno haya atakuwa amejitungia swali.**

**-Kisa kikubaliane na dondoo.**